

**HALMASHAURI YA MJI MBINGA**  
**KIKAO CHA BODI YA ZABUNI**  
**30.10.2021**

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao
2. Ombi la kupitia na kuridhia matumizi ya force account katika ujenzi wa madarasa na Mkandarasi katika Ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya-Kituo cha afya Kalembo.
3. Idhini ya kutangaza na kupitisha nyaraka za zabuni ya Ujenzi wa nyumba za watumishi wa Idara ya afya – Kituo cha Afya Kalembo
4. Mengineyo
5. Kufunga kikao

**MAHUDHURIO**

- |                    |        |
|--------------------|--------|
| 1. Joseph Mhagama  | M/KITI |
| 2. Shaban Mzee     | Katibu |
| 3. Shani G.Mhagama | Mjumbe |
| 4. Donald Msigwa   | Mjumbe |
| 5. Amon N. Sangana | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

- |                   |                      |
|-------------------|----------------------|
| 1. Jesse Shengena | Mjumbe – Kwa taarifa |
|-------------------|----------------------|

**SECRETARIET**

1. Hellen Harrison

**MTC/TB/MHT/09 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao Mnamo Saa 5:00 asubuhi na kuwakaribisha wajumbe

**MTC/TB/MHT/10 OMBI LA KUPITIA NA KURIDHIA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT KATIKA UJENZI WA MADARASA NA MKANDARASI KATIKA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUIMSHI KATIKA KITUO CHA AFYA KALEMBO**

Mwenyekiti alimwomba Katibu wa bodi ya zabuni kusoma mwongozo uliotoka OR-TAMISEMI ukitaka taasisi husika kutumia Force Account katika ujenzi wa madarasa ya mradi wa UVIKO 19 na matumizi ya Mkandarasi katika ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika kituo cha Afya Kalembo. Baada ya Katibu kuwasilisha , Wajumbe walijadili na kuridhia kutumia force Account katika ujenzi wa madarasa na Mkandarasi katika Ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika kituo cha Afya Kalembo.

**MTC/TB/MHT/11 OMBI LA IDHINI YA KUTANGAZA NA KUPITISHA NYARAKA YA ZABUNI YA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUIMSHI IDARA YA AFYA - KITUO CHA AFYA KALEMBO**

Katibu aliwasilisha ombi la kuanza mchakato wa kumpata Mkandarasi na pia aliwasilisha tangazo na kitabu cha zabuni kitakachotumika katika mchakato mzima wa Ujenzi wa Mradi huo ili wajumbe wa Bodi ya Zabuni wapitie na kutoa idhini ya

kuanza taratibu za manunuzi. Wajumbe walipitia tangazo na kitabu na kuridhia mchakato huo uanze mara moja kwani mwongozo ulioletwa ulikuwa na maagizo ya kufanyika kwa haraka ili kumpata Mkandarasi.

### **MTC/TB/MHT/12 MENGINEYO**

Hapakuwa na Mengineyo

### **MTC/TB/MHT/13 KUFUNGA KIKAO**


Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 05:45 asubuhi

**=UMETHIBITISHWA=**

(Katibu)

  
**Shaban Mzee**

Mwenyekiti)

  
**Joseph C Mhagama**